

Josephina Bakhita



Mtakatifu Josephina Bakhita,

uliuzwa katika utumwa ukiwa mtoto na ukavumilia mateso na ukatiri husiosemeka.

Baada ya kutoka katika utumwa, ulipata msingi bora wa wokovu kwa kumjua Yesu Kristu pamoja na kanisa lake.

Ee Mtakatifu Josephina Bakhita,

waokoe wale wote ambao wametekwa katika utumwa, uwaombnee kwa Mungu wa huruma, hili minyororo ya utumwa ikakatike na wakawe huru.

Mungu mwenyewe akawaponye na kuwafariji wale ambao wako katika mazingira hatarishi, wenyе majeraha ya roho na mwili yaliyo sababishwa na utumwa, na wale wote ambao wametendewa unyanya kupitia hii biashara ya utekaji wa binadamu.

Wape faraja wale ambao wamenusurika kutoka katika janga hili la utumwa, wafundishe kumtazama Yesu kama mfano wa Imani na Matumaini, hili wakaweze kupona majeraha yao.

Tunakuomba utuobee pia nasi, hili tufungue macho na kuweza kuona mateso na majeraha ya kaka na dada zetu, walionyimwa utu na uhuru wao, tujalie kusikia kilio chao na tuweze kuwasaidia.

Amina